

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegram "AFYA", DODOMA
Namabari ya Simu: +255 026 – 2323267



Mji wa Serikali Mtumba
Barabara ya Afya
S.L.P. 743,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI
Dodoma, Jumatano Aprili 15, 2020.

Kwa mujibu wa sampuli zilizopimwa katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii tarehe 14 na 15 Aprili, 2020, Wizara inatoa taarifa ya uwepo wa **wagonjwa (29)** waliothibitika kuwa na ugonjwa wa Corona (COVID-19) nchini. Wagonjwa hawa wote ni Watanzania, kati yao **ishirini na sita (26)** wapo Dar es Salaam, **wawili (2)** wapo Mwanza na **mmoja (1)** yupo Kilimanjaro na wote wanaendelea na matibabu chini ya uangalizi wa wataalam wa afya. Ufuatiliaji wa watu waliokuwa karibu na wagonjwa hawa unaendelea (Contact Tracing).

Hivyo hadi kufikia leo jumla ya **watu 88** wamepata maambukizi ya COVID-19 nchini kutoka **53** tuliowatolea taarifa awali. Ongezeko hili la wagonjwa linajumuisha wagonjwa wapya **sita (6)** waliotolewa taarifa na Waziri wa Afya wa Zanzibar mapema leo tarehe 15 Aprili, 2020. Aidha wagonjwa waliopona hadi leo ni **kumi na moja (11)**. Vifo vitokanavyo na COVID-19 nchini ni **vinne (4)**.

Serikali inaendelea kuwataka wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu kama tunavyowapatia taarifa na elimu mara kwa mara kupitia njia mbali mbali. Katika kipindi hiki ni muhimu kwa wananchi kuepuka misongamano na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima. Aidha niwasihi wananchi kuacha kutoa taarifa za upotoshaji juu ya ugonjwa huu kwa kuwa zinaweza kuzua taharuki katika jamii.

A handwritten signature in green ink, appearing to read 'Umyy Mwalimu'.

Umyy Mwalimu (Mb)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO